

East African Journal of Swahili Studies

eajss.eanso.org

Volume 6, Issue 1, 2023

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>

EANSO

EAST AFRICAN
NATURE &
SCIENCE
ORGANIZATION

Original Article

Athari Ya Viarudhi Vya Ekegusii Kwa Kiimbo Cha Kiswahili Mionganoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili

Christine Nyougo^{1*} na Prof. Peter Githinji, PhD¹

¹ Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100. Nairobi, Kenya

* ORCID ID: <https://orcid.org/0000-0002-0186-7728>; Barua pepe ya mawasiliano: cnyougo@gmail.com

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1564>

Tarehe ya Uchapishaji: IKISIRI

10 Novemba 2023

Istilahini Muhimu:

Lugha ya kwanza,
Lugha ya pili,
Trokee,
Wizani silabi,
Uhawilisho,
Viarudhi.

Makala hii inadhamiria kuonyesha athari ya viarudhi vya Ekegusii kwa matumizi ya kiimbo cha Kiswahili sanifu. Wasailiwa wetu ni wanafunzi wa shule tatu za upili zinazopatikana katika eneo la Kisii. Tulijikita katika nadharia ya Mennen (2015) ya ujifunzaji wa kiimbo katika lugha ya pili. Nadharia hii huchunguza matatizo ambayo wajifunzaji wa lugha ya kwanza hupata wakati wa kujifunza kiimbo cha lugha ya pili. Tumejikita kwa mantiki kuwa mtagusano baina ya lugha moja na nyingine huweza kuibua kufanana au kutofautiana kimatumizi katika uenezaji wa viimbo tofauti. Tumetumia mihimili minne katika uchanganuzi wa data tuliyopata nyanjani. Mhimili wa kimfumo unashughulikia vipengele vya kiarudhi katika lugha husika na usambazaji wake, mhimili wa utekelezaji unashughulikia utaratibu wa namna ambavyo vipengele mbalimbali vya kifonolojia vinavyotekeleza majukumu yavyo katika lugha husika. Mhimili wa ujirudaijunaangazia kiwango cha matumizi ya vipengele hivi vya fonolojia ambapo lugha hutofautiana katika kiwango cha matumizi ya vipengele vyake na mhimili wa kisemantiki unaoshughuklika maana inayopatikana kutokana na matumizi ya viarudhi husiaka. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumiwa katika kuteua wanafunzi wa vidato tofauti katika shule tatu teule na walimu wanaofunza Kiswahili katika shule hizo. Data yetu ilitokana na hojaji, mahojiano usomaji wa sentensi pamoja na kifungu ambacho kilikuwa na aina nne za viimbo ambapo wasailiwa walizisoma kwa sauti. Data ya ziada ilitokana na usomaji wa sentensi nane za Ekegusii zenye kiimbo cha taarifa, swali, amri na mshangao ambazo zilisomwa na walimu wanaozungumza Ekegusii kama lugha ya kwanza katika shule hizo tatu. Uchanganuzi wa data ulifanywa kupitia ufasili wa data ya hojaji, mahojiano na uchunzaji wa kushiriki. Matokeo tuliyopata yalibainisha kuwa uhawilisho wa viarudhi hivi kwa kiwango kikubwa huathiri matumizi sahihi ya kiimbo cha Kiswahili ambapo wasailiwa wa lugha ya kwanza hurudufu baadhi ya vipengele vya lugha hiyo katika kiimbo cha lugha ya pili. Matokeo haya pia yalidhihirisha kuwa maumbo ya silabi katika Ekegusii, shadda, toni na wakaa huathiri matumizi ya kiimbo cha Kiswahili sanifu.

APA CITATION

Nyango, C. N. & Githinji, P. (2023). Athari Ya Viarudhi Vya Ekegusii Kwa Kiimbo Cha Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili. *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), 468-482. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1564>.

CHICAGO CITATION

Nyango, Christine Nyango and Peter Githinji. 2023. "Athari Ya Viarudhi Vya Ekegusii Kwa Kiimbo Cha Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 468-482. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1564>.

HARVARD CITATION

Nyango, C. N. & Githinji, P. (2023) "Athari Ya Viarudhi Vya Ekegusii Kwa Kiimbo Cha Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 468-482. doi: 10.37284/jammk.6.1.1564.

IEEE CITATION

C. N. Nyango & P. Githinji "Athari Ya Viarudhi Vya Ekegusii Kwa Kiimbo Cha Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 468-482, Nov. 2023.

MLA CITATION

Nyango, Christine Nyango and Peter Githinji. "Athari Ya Viarudhi Vya Ekegusii Kwa Kiimbo Cha Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Nov. 2023, pp. 468-482, doi:10.37284/jammk.6.1.1564.

UTANGULIZI

Uelewa wa matamshi faafu katika lugha geni ni jambo gumu na ni watu wachache tu wanaofaulu kutamka kama wazawa wa lugha hiyo wakati wanapojojifunza lugha ya pili (L2) katika utu uzima (Mennen, 2015). Kipengele mojawapo ambacho watu hupata tatizo katika matamshi ni kiimbo. Wajifunzaji wengi wa lugha ya pili wanapozungumza katika lugha lengwa, kiimbo chao hutofautiana na kile cha wazungumzaji asilia. Hata baada ya miaka mingi katika utumiaji wa L2, tofauti hizi za matumizi ya kiimbo huchangia katika kutoimarika kwake katika lugha hiyo ngeni (Mennen, 2004). Jambo hili hudhihirika zaidi wakati athari za L1 zinajitokeza katika kiimbo cha L2, hasa katika viwango vya juu vya ustadi (Mennen, 2004; 2007).

Ujifunzaji wa matamshi bora ya Kiswahili kama L2 ni mchakato mrefu ambao una changamoto nyingi mionganoni mwa wanafunzi. Changamoto kubwa zaidi hutokana na athari ya lugha ya kwanza katika mazungumzo ya lugha pili. Aghalabu, mwanafunzi anayejifunza L2 huwa anao umilisi wa kutosha wa L1. Hivyo, mwanafunzi huyo huanza kujifunza lugha lengwa kuanzia kiwango cha chini ambapo huwa ana ustadi mdogo wa L2. Mjifunzaji huyo hukumbana na changamoto kuanzia pembejeo, mazingira ya ujifunzaji, nyenzo, hulka na mielekeo kuhusu lugha anayojifunza. Kuna baadhi ya mambo

ambayo mjifunzaji hudhibiti haraka kama msamiati wa kimsingi na vipengele vya mawasiliano sahili kama vile salamu, kuagana na kuomba maelekezo, ilhali masuala mengine kama vile sarufi changamano na matamshi bora huchukua muda.

Athari zinazotokea jamii moja inapajaribu kujifunza L2 zimehusishwa na uhawilisho wa vipengele vya L1 hadi L2 (Vâlcea, 2020). Kwa mujibu wa Corder (1967), L1 huathiri L2 mtu anapojojifunza kabla ya kuzoea matumizi na kanuni za L2. Athari hizi hubainika katika viwango vingi zaidi wakati L1 na lugha lengwa zinatofautiana kumuundo; hata hivyo, lugha zeny ukuruba wa kumuundo kama Kiswahili na Ekegusii ambazo ni za Kibantu zinaweza kutofautiana katika baadhi ya vipengele. Kiswahili kinachozungumzwa katika kaunti ya Kisii mionganoni mwa wanafunzi wenyе asili ya Gusii waliozaliwa na kulelewa sehemu za vijijini kwa mfano, kina upungufu wa ufasaha kimatamshi hasa katika matumizi ya kiimbo.

Tafiti zilizofanya kama vile Khvtisiashvili (2018), aliyechunguza namna mjifunzaji wa lugha ya pili katika hatua za kwanza, hutumia sheria za fonolojia ya L1 katika matamshi yake ya L2 na Obara (2014) aliyetafiti kuhusu makosa ya matamshi katika Ekegusii zimeonyesha namna L1 inavyoathiri L2 katika viwango mbalimbali, kutoka vipandesauti huru hadi kiwango cha

diskosi. Makala hii ilijikita katika suala la kiimbo kwa sababu ni mojawapo ya sifa za kiarudhi. Tumejikita katika suala la athari za kiimbo cha Ekegusii kwa Kiswahili kwa sababu suala la jinsi Ekegusii inavyoathiri kiimbo cha Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za upili bado halijafanyiwa utafiti wa kiusomi. Kutokana na kutambua kuwa Kiswahili na Ekegusii zina mifumo tofauti ya viarudhi, kuna haja ya kuchunguza athari za Ekegusii zinavyojitokeza kwa wanafunzi wa Kiswahili ambaa lugha ya kwanza ni Ekegusii. Hili latokana na kuwa kutokuwepo kwa baadhi ya viarudhi vingine vinavyopatikana katika Ekegusii kama vile toni huathiri kiimbo katika lugha ya Kiswahili na pia kutathmini jinsi usuli na tajriba ya wanafunzi husababisha tofauti katika kiimbo wakati wa kuzungumza Kiswahili. Makala hii inajikita katika fonolojia arudhi na vipengele ambavyo tutakuwa tukishughulikia ni toni, wakaa, silabi na shadda. Ni katika utekelezaji wa vipengele hivi wakati wa utamkaji wa kiimbo ambapo tunapata tofauti za kimaana katika aina nne za sentensi ambazo ni taarifa, swali, amri na mshangao.

MISINGI YA NADHARIA

Nadharia ya ujifunzaji wa kiimbo katika lugha ya pili (NUKL2) ya Mennen (2015) huchunguza matatizo ambayo wazungumzaji wa lugha ya kwanza hupata wakati wanapojifunza kiimbo cha lugha ya pili. Huonyesha namna tofauti katika matumizi ya kiimbo hupungua na hata kutoweka kadiri ustadi katika matumizi unavyoongezeka. Huonyesha iwapo kuna mipaka katika utamkaji wa kiimbo katika ujifunzaji mionganoni mwa wajifunzaji wa mazingira tofauti, na namna ambavyo mitindo ya uzungumzaji inavyoweza kuathiri kiimbo katika viwango mbalimbali vya ustadi. Nadharia hii kwa mujibu wa Mennen (2015) ina mihimili ifuatayo:

- Kipengele cha kimfumo: Idadi ya vipengele vya kifonolojia (wakaa, kidatu, toni na kiimbo) na usambazaji wake. Hushughulikia kuwepo au kutokuwepo kwa vipengele vya kiarudhi katika L1 na L2 na jinsi utaratibu wa kupanga vipengele hivi unaweza kutofautiana

mionganoni mwa watumiaji wa lugha hizo. Wazungumzaji wa L2 kwa mfano, wanawenza kupuuza toni ya lafudhi fulani ambayo huenda ikatokea katika L2 kutokana na kutokuwepo kwa toni hiyo kana kiarudhi cha L1 yao.

- Kipengele cha utekelezaji: Utaratibu wa namna ambavyo vipengele mbalimbali vya kifonolojia vinavyotekeleza majukumu yavyo. Lugha zinawenza kuwa na vipengele vya kiarudhi vinavyofanana, lakini kwa lugha moja, mpandoshuko ukaanza au kuishia mahali tofauti na lugha nyingine, au zote zinakuwa na wakaa, lakini moja ikawa na wakaa mrefu na nyingine ikakosa wakaa mrefu.
- Kipengele cha ujirudiaji: Kiwango cha matumizi ya vipengele hivi. Lugha hutofautiana katika kiwango cha matumizi ya vipengele vyake. Lugha mbili zinawenza kuwa na vipengele sawa lakini lugha moja ikavutumia kwa kiwango cha juu kuliko ile nyingine
- Kipengele cha maana: Uamilifu wa vipengele hivi katika kuleta maana. Kufanana au kutofautiana katika kipengele cha maana huhusisha matumizi ya vipengele au midundo inayopitisha maana kwa mfano, lugha inaweza kuwa tofauti kwa namna inavyozingatia au kuonyesha kuuliza swali, taarifa, kuamrisha au mshangao.

Nadharia hii pia imetumiwa na Mennen et al. (2022) katika kuchanganua usimilikaji wa athari za viarudhi vya L2 kwa L1 ya wazungumzaji. Waligundua kuwa athari za L2 zinawenza kupatikana kwa L1, jambo ambalo ni kinyume na imani ya wengi kuwa ni L1 pekee ambayo huathiri L2. Son (2018) pia ameitumia nadharia hii katika kuchunguza upataji wa kiimbo cha lugha ya pili (Kihispania) mionganoni mwa wazungumzaji wa Kikorea kama L1. Matokeo yake yalionyesha kuwa lafudhi ya Kikorea inaathiri kiimbo mionganoni mwa walio katika hatua za mwanzo za ujifunzaji ikilinganishwa na wale ambaa wamejifunza kwa muda mrefu. Pia alibainisha

kuwa wazungumzaji asili wa Kikorea walikuwa na tatizo katika kuonyesha mipaka ya toni kakika lugha ya Kihispania. Makala hii itajikita katika mhimili hii minne katika kuchanganua sentensi nane zilizosomwa na wasailiya mbalimbali ili kuchambua tofauti inayojitokeza katika vipengele vya shadda, toni, na wakaa baina ya Ekegusii na Kiswahili na athari yake kwa kiimbo cha Kiswahili. Tofauti katika utamkaji wa viarudhi kati ya Ekegusii na Kiswahili itafasiliwa kwa mujibu wa mhimili wa utekelazaji ilhali urudufu wa viarudhi vya Ekegusii wakati wa kutumia kiimbo cha Kiswahili utafasiliwa katika muktadha wa muhimili wa ujirudiaji. Kuwepo kwa viarudhi katika Ekegusii ambavyo havipo katika Kiswahili kutachukuliwa katika muktadha wa mhimili wa kwanza ilhali matatizo ya kimaana yanayotokea mionganini mwa wasailiya katika ufasili wa aina nne za sentensi kumejikita katika mhimili wa semantiki.

MBINU ZA UTAFITI

Data iliyotumika katika Makala hii tuliipata kuititia njia mbili kuu: uchunguzi wa maktabani uliojumuisha usomaji wa vitabu, tasnifu na Makala mbalimbali kuhusu viarudhi, nadharia pia ilioongoza uchunguzi huu. Ukusanyaji wa data ulitumia vifaa kama vile; hojaji, mahojiano, uchunzaji wa kushiriki pamoja na kinasa sauti cha simu. Data ya maktabani na nyanjani iliunganishwa ili kuoanisha maoni ya wasomi. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo na michoro. Data ya nyanjani ilitoka kwa hojaji, mahojiano, usomaji wa aina nne za sentensi kwa Kiswahili, usomaji wa kifungu chenye aina nne za sentensi na pia usomaji wa aina nne za sentensi kwa Ekegusii. Wasailiya waliteuliwa kutoka shule tatu za upili ambazo ni: Senior Chief Musa Nyandusi, Nyamondo, na Nyabisia ambazo zinapatikana katika Kaunti ya Kisii nchini Kenya. Shule hizi ziliteliwa kimaksudi kwa vile zinawakilisha maeneo tofauti ya gatuza ndogo za Kisii zilizo na wazungumzaji wenye lahaja mbili tofauti za Ekegusii. Shule ya Nyabisia ina wazungumzaji wa Ekerogoro ambayo inaaminika kuwa ndiyo lahaja sanifu ya Ekegusii na inatumika katika maandishi mengi ya Ekegusii,

hata katika vyombo vya habari vinavyotangaza kwa Ekegusii. Shule ya Nyamondo ina wazungumzaji wa Ekemaate lahaja inayochukuliwa kuwa si sanifu, nayo shule ya Senior Chief Musa Nyandusi ina wazungumzaji wa Ekegusii wanaotoka mjini na vijiji, hivyo zinawakilisha kaunti nzima ya Kisii. Wanafunzi walioshirikishwa ni wa kidato cha kwanza, pili na tatu. Kwa upande mwengine walimu waliohusishwa ni wale wanaofunza Kiswahili katika shule hizi tatu zilizotajwa.

Wanafunzi 129 walihuushwa katika kujaza hojaji ambapo walipaswa kutaja usuli wa lugha za kwanza pamoja na eneo wanaloetoka, Pia walismewa sentensi zilizokuwa katika hojaji na mtafiti ambapo walihitajika kujaza aina ya sentensi iliyosomwa yaani: taarifa, swali, amri au mshangao. Kupitia uteuzi wa kimaksudi katika vikundi, wanafunzi kumi na wawili waliteuliwa ambapo walipewa sentensi za taarifa, maswali, amri na mshangao na kuombwa kuzisoma katika kuchunguza iwapo waliweza kutumia kiimbo kwa njia sahihi katika usomaji wao. Baadaye wanafunzi hawa walipewa kifungu cha maneno sitini na sita (66) na kuombwa kusoma ili kuona iwapo waliweza kutumia kiimbo sahihi katika usomaji wao wa sentensi mfululizo. Kila msailiwa alihitajika kusoma kifungu hicho kwa sauti huku akidhihirisha aina mbalimbali za viimbo vilivyokuwa katika kifungu. Pia tulitumia mbinu ya mahojiano kwa walimu kuhusu namna ambavyo wao hufunza kiimbo cha lugha ya Kiswahili. Pia walihuushwa katika utoaji wa data ya ziada kwa kusoma sentensi za Ekegusii na tafsiri yazo katika lugha ya Kiswahili ili kudhihirisha viarudhi vingine vya Ekegusii kama vile shadda, toni na wakaa. Kabla ya kuwasilisha matokeo ya utafiti, tutaanza kwa kutoa muhtasari wa tofauti kati ya maumbo ya silabi za Ekegusii tukitilia maanani kuwa kuna ukuruba mkubwa kati ya maumbo ya silabi za Ekegusii na Kiswahili.


Tofauti ya Maumbo ya Silabi za Ekegusii na Kiswahili

Vokali ndicho kipashio cha kimsingi katika silabi za lugha za binadamu ikiwatuwa na kuwepo au

kutokuwepo kwa konsonanti. Kwa mujibu wa Nash (2011), kina katika silabi za Ekegusii hakigawanyiki na hakuna uwezekano wa kuwepo koda kwa kuwa kila silabi ya lugha hii huishia kwa vokali. Pia sehemu ya kilele lazima iwe na mora moja na isizidi mbili. Sehemu ya tangulio katika lugha ya Ekegusii inaweza kuwa na miundo ifuatayo: konsonanti, konsonanti ya unasalishaji, konsonanti na kiyeyusho na kiyeyusho (Beale-Rivaya, 2022). Mose (2020) alibainisha kuwa lugha ya Ekegusii ina muundo wa silabi unaopendelewa wa vokali (V) au wa konsonanti vokali (KV), ingawa katika mazingira fulani huweza kuwa na muundo wa konsonanti kiyeyusho na vokali (KYV). Lugha ya Ekegusii haikubali mwambatano wa konsonanti. Pale

ambapo pana sauti za nazali tangulizi, hili huchukuliwa kama tamko moja, yaani konsonanti inayonazalishwa, badala ya mwambatano wa konsonanti mbili. Ilhali Kiswahili kinaruhusu silabi za konsonanti pekee ambapo nazali huwa kwenye kilele cha silabi (Nandelenga, 2015), hakuna uwezekano wa kuwepo kwa nasali kwenye kilele cha silabi katika Ekegusii, bali nasali hujumuishwa na konsonanti nyingine inayowekwa katika sehemu ya tangulio. Tofauti nyingine kati ya lugha hizi mbili katika muundo wa silabi ni kuwa Ekegusii kina irabu ndefu ambayo huchukuliwa kuwa na mora mbili ilhali irabu ndefu katika lugha ya Kiswahili inaweza kuwa na silabi mbili huku kila moja ikiwa na mora moja kama inavyoonyeshwa katika kielelezzo 1.

Kielelezzo 1: Uwakilishaji wa kipashio cha kiarudhi [sa:] katika Kiswahili na Ekegusii



Mfano wa (a) hapo juu unawakilisha kipashio cha kiarudhi katika Kiswahili ambacho badala ya kuwa sibabi moja yenyе mora mbili zinakuwa silabi mbili nyepesi, kila moja ikiwa na kina chake. Umbo lilo hilo katika Ekegusii linaonyesha silabi moja nzito yenyе mora mbili. Tofauti hii inatokana na kuwa silabi ya Kiswahili haizingatii wizani silabi, yaani hakuna silabi yenyе irabu ndefu kama inavyobainishwa na Ntihirageza (2001) na Mwaliwa (2014). Hali hii ndiyo inafanya jozi mizani katika lugha ya Kiswahili

kuwa ya trokee silabi, kumaanisha kuwa shadda huwekwa kwa sibabi ya kwanza kwa kila jozi mizani. Kwa upande mwingine, jozi mizani katika Ekegusii ni ya trokee mora, kumaanisha kuwa shadda inawekwa kwa mora ya kwanza katika jozi mizani. Tofauti hii itakuwa na athari katika kiimbo cha maneno kwa sababu tofauti ya vipengele vya kiarudhi na jinsi vinavyotekelozwa katika lugha hizi mbili kutafanya wazungumzaji wa Ekegusii warudufu ruwaza za Ekegusii na vilevile kufasiri semi za Kiswahili kwa njia yenyе

dosari. Maelezo haya kuhusu tofauti za miundo ya silabi kati ya lugha hizi mbili ni muhimu kwa sababu silabi ni kipashio muhimu sana katika kuchanganua arudhi za lugha yoyote ile. Katika makala yetu tutaangazia baadhi ya viarudhi hivi tukianza na shadda.

MATOKEO NA MAJADILIANO YA MATOKEO

Shadda katika Ekebusii na Athari Yake kwa Kiimbo cha Kiswahili

Shadda au mkazo ni utaratibu wa utamkaji neno ambapo silabi moja hutamkwa kwa nguvu nydingi zaidi kuliko zingine katika neno husika (Kihore na wenzake, 2008; Massamba, 2012). Lugha za Kibantu hutumia shadda tuli (Barlow, 1960) ambayo huwekwa kwenye silabi maalum katika neno. Kila lugha ina utaratibu wake wa kuweka shadda katika neno ambao kwa kawaida unaweza kutabirika. Mgullu (1999) anadai kuwa lugha nydingi hubainisha viwango viwili vya shadda: neno na sentensi. Aina ya kwanza hutokea wakati nguvu huwekwa kwenye silabi mojawapo katika neno husika. Kulingana na Osinde (1988), shadda msingi katika Ekebusii huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho wa neno. Goldsmith (1990) amedai kuwa katika lugha nydingi za binadamu, shadda katika maneno yanayoundwa kwa silabi moja huangukia vokali katika neno hilo. Katika lugha ya Ekebusii shadda katika maneno yanayoundwa kwa silabi moja huwekwa kwenye vokali ya silabi hiyo kama anavyodai Goldsmith. Kwa upande mwingine, maneno yanayoundwa kwa silabi mbili au zaidi huwekewa shadda kutegemea miundo ya maneno hayo. Katika kitenzi *rema* ‘lima’ kwa mfano, Shadda huwekwa katika silabi [re]. Hii ni kwa sababu maneno ya Ekebusii yaliyo na silabi mbili huwekwa shadda katika silabi ya pili kutoka mwisho kama anavyodai Osinde (1988), kama ilivyo katika Kiswahili. Tukitumia mhimiili wa utekelezaji wa NUKL2 (Mennen, 2015), hatupati tofauti kati za lugha hizi mbili katika uwekaji wa shadda kwenye maneno mbalimbali. Hata hivyo, kwa kuwa kiimbo hubainika katika kiwango cha sentensi, tunaangazia zaidi kipashio cha sentensi hasa kwa sababu mkazo unaowekwa kwenye sentensi ndio

unaaoathiri maana tukizingatia muhimili wa semantiki. Shadda sentensi huwekwa mahali fulani kwenye sentensi na hupatikana katika silabi fulani ya maneno yanayoiunda. Ili kubaini namna shadda huwekwa katika sentensi za Ekebusii tulitumia uchunzaji wa kushiriki ambapo tuliwapa walimu wanne sentensi nane za Ekebusii ambazo baadaye zilitafsiriwa hadi Kiswahili kwa mujibu wa ulinganishaji.

Data 1

1. Omwana ngosoma are egetabu.
Mtoto anasoma kitabu.
2. Notagete komanya eri eta riaye?
Unataka kujua jina lake?
3. Omoibi oria ochandire abanyakenyoro!
Mwizi yule amewasumbua wanakijiji!
4. Igoro ntwasimegete chi bando mogondo!
Jana tulipanda mahindi shambani
5. Rema omogondo bwonsi rero
Limeni shamba lote leo!
6. Endagera enyansu yayiire bono iga?
Chakula kitamu kimeiva saa hizi?
7. Genda orie endagera yao
Nenda ukale chakula chako!
8. Embura yabogoirie ebimeri bionsi!
Lo! Mvua imebeba mimea yote!

Katika sehemu inayofuata, tutatumia NUKL2 (Mennen, 2015) kuchambua tofauti katika uwekaji wa shadda katika sentensi hizi za Ekebusii. Tutaangazia tofauti iliyopo baina ya Ekebusii na Kiswahili katika uwekaji wa sadda katika sentensi za taarifa, swalii, amri na mshangao. Ni kutokana na ulinganishaji wa tofauti katika uwekaji shadda kati ya lugha hizi mbili ambapo tutaelewa athari za mfumo wa

viarudhi nya Ekegusii kwa matamshi faafu ya kiimbo cha Kiswahili mionganoni mwa wanafunzi wanaozungumza Ekegusii kama L1.

Sentensi za Taarifa

Sentensi (1) na (4) katika kikoa cha (1) hapo juu ndizo tulizotumia kama sentensi za taarifa katika (2) hapa chini. Katika kusoma sentensi “Omwana ngosoma are egetabu” *Mwanafunzi anasoma kitabu* na “Igoro ntwasimegete chi bando mogondo!” *Jana tulipanda mahindi shambani*, wasailiwa wote waliweza kusoma ifaavyo. Kuna tofauti ndogo inayodhihirika katika uwekaji wa shadda katika sentensi za Ekegusii na visawe vyake nya Kiswahili kama ifuatavyo katika data (1)

Data 2

1. O'mwana 'ngosoma 'are e'getabu
Mwana'funzi ana'soma ki'tabu
2. I'goro n'twasimegete chi 'bando mo'gondo

'Jana tuli'panda ma'hindi sha'mbani.

Katika Ekegusii, sentensi zilizosomwa na wasailiwa zinaonyesha kuwa shadda iliwekwa katika silabi ya kwanza ya kila neno ingawa viambishi awali havikuwekwa shadda hata vikitokea kama silabi ya kwanza. Ilhali shadda ya Kiswahili itasalia katika silabi ya pili kutoka mwisho, shadda ya Ekegusii inaonekana kubadilikabdalika kwa maneno yenye zaidi ya silabi mbili. Shadda katika sentensi inaweza kutokea katika maneno mbalimbali kulingana na nia ya msemajji, yaani kile anachotaka kusisitiza. Hata hivyo, kwa kawaida katika sentensi za taarifa, shadda inapatikana katika kitenzi. Hivyo basi, tutaipata katika maneno ‘anasoma’ na ‘tulipanda’ ikiwa tutataka kusisitiza tendo. Katika Ekegusii, wasailiwa pia waliweka shadda katika vitenzi ‘ngosoma’ na ‘ntwasimegete’. Huenda kuwa kufanana huku katika kategoria ya maneno yanayowekwa shadda za sentensi kwa mujibu wa mhimiili wa mfumo wa NUKL2 kulikuwa na athari chanya katika utamkaji wa kiimbo cha

Kiswahili kwa sentensi za taarifa. Hata hivyo, kulikuwa na tofauti ndogo iliyokuwa katika nomino zilizo na viambishi ambazo hazikuwekwa shadda kwenye silabi ya pili katika Ekegusii.

Sentensi za Swalii

Kutokana na data katika (1) hapo juu, sentensi mbili za maswali ni sentensi (2) “Notagete komanya eri eta riaye” *Unataka kujua jina lake?* na sentensi (6) “Endagera engiya yayiire bonoiga” *Chakula kitamu kimeiva saa hizi?* Uwekaji wa shada unadhihirisha tofauti katika Ekegusii na Kiswahili

Data 3

2. 'Notagete 'komanya eri 'eta 'riaye?
Una'taka ku'jua 'jina 'lake?
6. E'ndagera e'ngiya yayi'ire 'bonoiga?

Cha'kula ki'tamu kime'iva 'saa 'hizi?

Kama tulivyotaja hapo awali, shadda ya Kiswahili inapatikana katika silabi ya pili kutoka mwisho kwa kila neno kama inavyoonyeshwa katika sentensi (2) na (6). Katika visawe vyake nya Ekegusii, wasailiwa waliweka shadda katika silabi ya kwanza ya maneno huku viambishi awali vikikosa kushirikishwa katika uwekaji wa shadda. Kwa mfanu, katika neno ‘e'ndagera’ shadda haipo katika silabi [e] ambayo ni kiambishi cha umoja. Katika uwekaji wa shadda katika sentensi za swalii, Kiswahili hutilia mkazo neno la mwisho, lakini katika Ekegusii, mkazo uko katika virai vinavyotokea mwisho wa swalii katika ‘erjeta riaye’ na ‘bonoiga’ badala ya kwenye maneno ya mwisho. Tukijikita kwa muhimili wa mfumo na utekelezaji, katika nadharia ya ujifunzaji wa kiimbo cha lugha ya pili (NUKL2) ya Mennen (2015), lugha ya Ekegusii huwa na matumizi tofauti ya kiimbo cha swalii ikilinganishwa na Kiswahili. Katika ya wasailiwa wanne tulio wahusisha katika usomaji wa sentensi za Kiswahili, watatu walisoma vizuri ingawa mmoja hakuweza kusoma vizuri kwa kuwa aliweka mkazo katika kila neno bila kuelewa kuwa katika

kiimbo cha swalii, sauti hupanda katika neno la mwisho (Massamba, 2012). Inaonekana kuwa msailiwa huyu alitativika kufanya maamuzi iwapo arudufu ruwaza za Ekegusii au afuate ruwaza ya Kiswahili. Suluhu lake laonekana kuegemea ile dhana ya ujirekebishihi unaokiuka viwango vya kawa (Labov, 1966; Janda & Auger, 1992) amba hutokana na juhudzi za mzungumzaji za kujaribu kufuata kaida dhanifu za matumizi ya lugha. Hata hivyo, ni vizuri kutilia maanani kuwa ufasili sahihi wa sentensi za swalii kwa kiwango kikubwa kama ilivyodhihirishwa katika utafiti wetu unaashiria kuwa hakuna tofauti kubwa kati ya semantiki ya swalii katika lugha hizi mbili kama inavyobashiriwa na mhimili wa kisemantiki wa nadharia ya uwekaji kiimbo katika lugha ya pili.

Sentensi za Amri

Uchambuzi wa sentensi za amri ulilenga sentensi (5) Rema omogondo bwonsi rero! *Limeni shamba lote leo!* na sentensi (7) Genda ori endagera yao! *Nenda ukale chakula chako!* Ambazo zimewasilishwa katika (4) hapo chini. Katika sentensi za Kiswahili, kiimbo cha amri hutamkwa kwa kuweka mkazo katika neno la kwanza. Hivyo basi, wahuksika walipaswa kusoma sentensi hizi kwa kiimbo cha juu (kinachopanda), huku wakiweka mkazo katika neno “limeni” na “nenda”. Hata hivyo, wasailiwa wawili kati ya wanenye ndio waliosoma ifaavyo ilhali wawili hawakuweza kusoma kwa kiimbo sahihi cha Kiswahili kwa kuwa hawakuweza kuweka shadda mahali panapofaa. Hebu tutazame mifano ya Ekegusii ili tuone jinsi shadda ilivyowekwa na wasailiwa katika maneno husika.

Data 4

- 5. **'Rema omo'gondo 'bwonsi 'rero'!**
'Limeni shamba lote leo!
- 7. **'Genda 'ori e'ndagera 'yao'!**
'Nenda ukale chakula chako!

Katika tafsiri ya Kiswahili shadda sentensi iko katika maneno “limeni” na “nenda”. Maneno ‘limeni’ na ‘nenda’ pia yana shadda katika silabi ya pili kutoka mwisho, yaani silabi ‘me’na ‘ne’ mtawalia. Katika Ekegusii, badala ya shadda

sentensi kuwa katika neno la kwanza, iko katika vishazi vitenzi ‘rema omogondo’ na ‘genda ori’. Kwa mujibu wa kipengele cha utekelezaji katika NUKL2, lugha au makundi ya L1 huweza kutofautiana pakubwa katika matumizi na L2. Tofauti hii ya uwekaji wa shadda katika sentensi ya Ekegusii na Kiswahili huenda ndiyo huleta tatizo katika utamkaji wa kiimbo sahihi cha Kiswahili sanifu kutokana na kuwa urudufu wa ruwaza za L1 katika kipengele cha ujirudiaji wakati wa kutumia L2 kunasababisha ruwaza za L1 kujitokeza katika L2.

Usomaji wa Sentensi ya Mshangao

Sentensi za mshangao zinazoangaziwa kutoka mifano iliyoko katika (1) hapo juu ni namba (3) na (8) za Kiswahili na visawe vyake katika Ekegusii kama vilivyoordheshwa katika (5) hapo chini. Kiimbo cha mshangao katika lugha ya Kiswahili hupanda na kushuka katika silabi ya mwisho katika neno la mwisho (Massamba, 2012) kama ilivyodhihirishwa katika (3) na (8).

Data 5

- 3. 'Mwizi 'yule amewasu'mbuwanaki''jiji!

Omo'ibi o'ria o'chandire abanyake'nyoro!

- 8. Lo! M'vua ime'beba mi'mea 'yote!

Obee! e'mbura yabo'goirie ebi'meri bi'onsi!

Matokeo yalidhihirisha kuwa shadda iliwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho wa neno katika lugha zote mbili isipokuwa katika Ekegusii, maneno yaliyokuwa na vitenzi vya zaidi ya silabi mbili kama vile ‘yabo’goirie’, shadda iliwekwa katika silabi ya nne kutoka mwisho. Katika sentensi hizi mbili, kiimbo cha Kiswahili kinafaa kiwe katikati ya ‘ji’ mbili katika sentensi 3 na kati ya ‘yo’ na ‘te’ katika sentensi 8. Kwa upande mwingine usomaji wa sentensi za Ekegusii uliathihiriwa na matumizi ya shadda sentensi katika virai nomino mathalani ‘ebimeri bionsi’ na wala si ‘bionsi (yote) namna ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Haya yanabashiriwa na mhimili wa utekelezaji wa NUKL2 unaohusu kuweko kwa

ruwaza tofauti za utekelezaji wa matamshi. Huenda hali hii ndiyo ilitatiza wasomaji katika uwekaji wa kiimbo sahihi cha Kiswahili hivyo kuathiri matokeo kuhusu utamkaji wa sentensi ya mshangao ambapo baadhi ya wasailiwa walitafsiri kama taarifa, amri na hata swali. Vilevile, tukirejelea mhimili wa mfumo, tutapata kuwa tofauti ya vipengele vya arudhi baina ya L1 na L2 inapunguza athari chanya ambazo zingesaidia katika matumizi bora ya kiimbo cha lugha lengwa. Katika muktadha huu tunaweza kutoa madai kuwa hata kama kwa kiwango kikubwa Kiswahili na Ekegusii huweka shadda katika silabi ya pili ya neno, vitenzi vya Ekegusii pamoja na virai nomino vinavyoikiuka kanuni hii pamoja na matumizi ya virai vya Ekegusii katika uwekaji wa shadda, huathiri utamkaji wa kiimbo katika Kiswahili sanifu.

Toni katika Ekegusi na Kiimbo cha Kiswahili

Toni ni kipashio cha kiisimu ambacho hutumia kidatu katika kutofautisha maana za maneno (Yip, 2002). Kwa kawaida, kidatu hutegemea kupanda na kushuka kwa sauti (Massamba, 2012; Hyman, 1975; Roach, 1983). Kama kipande sauti huru, toni huwekwa katika rusu tofauti na vipande sauti, hivyo kipande sauti kikiwa katika rusu moja, kila kipande sauti huru huwa kwenye rusu tofauti.

Kielelezo 2: Mpangilio tofauti wa toni katika neno igoro

Rusu msingi	i	go	ro	i	go	ro
Rusu toni	JU	CH	CH	CH	JU	JU

Chanzo: Mogaka, 2009

Silabi tatu katika neno ‘igoro’ likiwakilishwa na toni ya JU-CH-CH huleta maana ya ‘juu’ na likiwa na toni ya CH-JU-JU huleta maana ya ‘jana’. Katika mfano huu, fonimu zote ziko sawa lakini toni ndiyo inayotofautisha leksia hizi. Kwa mujibu wa Welmer (1973), kuna jozi za maneno zenye mlinganuo finyu unaoletwa na toni.

Mstari huchorwa kuonyesha uhusiano wa vibeba toni na vipande sauti husika (Durand, 1990). Toni inaweza kuwa ya chini (CH) au ya juu (JU). Ekegusii ni lugha-toni ambayo hutumia ruwaza za kidatu ili kuleta tofauti za kileksia (Beale-Rivaya, 2022). Kiarudhi hiki huwakilisha dhana zifuatazo: nyakati mbalimbali katika vitenzi, umiliki, ukashaji na hata kategoria mbalimbali (Beale-Rivaya 2022; Mogaka, 2009). Kiarudhi hiki pia katika lugha hii huweza kutumiwa kuwatofautisha wazungumzaji wa lahaja ya Ekerogoro na Ekemaate. Nash (2011) anatambua aina tatu za toni katika lugha ya Ekegusii: (i) juu (ii) chini (iii) kushuka. Anabainisha kuwa toni ya kushuka hupatikana katika vokali ndefu pekee hivyo haibainiki sana kama ilivyo toni zingine kwa kuwa hali hii huchukuliwa kama kutumia toni ya juu na chini. Toni hubainika katika neno huku vokali ikiwa ni kipashio kidogo kinachobeba toni hiyo. Jukumu kubwa la toni katika lugha ya Ekegusii ni kuonyesha tofauti katika leksimu. Kupitia njia hii, maana za maneno yaliyoundwa kwa fonimu zilizo sawa katika mpangilio wazo hutofautishwa kupitia kwa toni ambapo utamkaji hudhihirika. Maana mbili za neno “igoro” zimeonyeshwa katika (6) hapa chini.

Data 6

Konsonanti na vokali katika maneno hayo hufanana ila tofauti hutokea katika toni pekee. Mifano ya seti za maneno mawili yanayoonyesha tu tofauti katika toni ni kama ilivyoonyeshwa hapo chini katika data (7)

Data 7

- i. Ntòmè- nitume mimi (nafsi ya kwanza
Ntómé-nitume (labda kitu alichonacho anafaa akitume)
- ii. Nkùnè- uniguse mimi
Nkúné- mimi niguse
- iii. Tògànyè- tungojee sisi
Tógányé- sisi tuwangoje
- iv. Tòròrè- nyinyi mtuone sisi
Tóróré – sisi tuwaone
- v. Bächwàtè-mwachape

Bächwáté- wao wachape

Data katika (7) zinaonyesha kuwa kila neno la kwanza katika nambari i-v lina toni ya chini. Kwa upande mwingine, imeonyeshwa kuwa lile la pili katika nambari i-v lina toni ya juu. Mifano hii inaweza kudhihirishwa kwa mlinganuo ufuatao kuonyesha mabadiliko katika maana

N tò mè - nitume mimi (nafsi ya kwanza)

CH CH N tó mé -nitume (labda kitu alichonacho anafaa akitume)

Mbali na kuleta maana tofauti ya neno, toni pia hutofautisha nyakati na hali katika lugha ya Ekegusii. Neno “ochire” linaweza kuwakilisha njeo tofauti kuegemea mpangilio wa toni za Kati (KA), Juu (JU) na Chini (CH) kama ilivyoonyeshwa katika (8).

Data 8

- Ōchírè (KA JU CH)-ameenda saa hizi.
- Ōchírè (KA JU CH) - ameenda saa hizi
- ōchíré (KA JU JU) - ameenda kitambo sana
- ōchíré (KA KA JU) - ameenda (hali timilifu)
- ōchíré (KA KA CH) - amekuja.

Usuli huu kuhusu toni utusaidia kuchambua athari za toni ya Ekegusii kwa kiimbo cha Kiswahili huku tukiangazia uwekaji toni katika maneno yaliyoko kwenye sentensi za amri na mshangao katika Ekegusii. Haya yanatokana na kuwa utafiti wetu uulionyesha kuwa wasailiwa walitatizika zaidi katika utamkaji na ufasili wa senetnsi za amri na zile za mashangao. Baadaye, tutalinganisha na kiimbo kilivyobainika katika visawe vya sentensi hizo katika Kiswahili. Katika kuchunguza iwapo toni katika lugha ya Ekegusii huathiri kiimbo cha Kiswahili, tuliafikiana na maoni ya wasomi kuwa Kiswahili hakina toni (Massamba 2012; Batibo, 2017). Sentensi zilizotumika ni zile zilizosomwa na walimu wanne kwa Ekegusii.

Sentensi za Amri na Mshangao

Sentensi (5) na (7) kutoka zile zilizoorodheshwa katika (1) zimechananuliwa ili kuangazia athari ya toni kwa sentensi za amri, nazo sentensi (3) na (8) zitawakilisha sentensi za mshangao.

Data 9

Mwizi yule amewasumbua wanakijiji!

Omoibi oria ochandire abanyakenyoro!

Rema omogondo bwonsi rero!

Limeni shamba lote leo!

Genda orie endagera yao!

Nenda ukale chakula chako!

Lo! Mvua imebeba mimea yote!

Obee! embura yabogoirie ebimeri bionsi!

Kila neno katika sentensi za (9) hapo juu lina silabi zilizo na toni. Tumekwisheseleza awali kuwa toni katika Ekegusii huwekwa katika kila silabi. Kuweko kwa mchanganyiko wa toni za juu, chini na kati kunafanya sentensi ziwe na mabadiliko mengi katika michakato ya vipengele vya kiarudhi. Katika sentensi za Kiswahili za kuamrisha kwa mfano, kiimbo huanza kwa sauti ya juu na kuendelea kushuka. Neno la kwanza

pekee ndilo linatamkwa sauti ikiwa imepanda huku kiimbo kikishuka katika maneno yanayofuata, lakini kutokana na kuweko kwa toni katika Ekegusii, kutakuwa na mpando-shuko katika silabi mbalimbali katika sentensi ya amri. Hali hii inatokana na kauli kuwa sentensi za amri aghalabu hutumia toni ya juu kwenye silabi moja katika kila neno kwenye sentensi. Sentensi za mshangao katika Kiswahili kunahitaji kushusha nguvu za utamkaji katika silabi ya mwisho, lakini Lugha ya Ekegusii itakuwa na sehemu nyingi zenyne kupanda na kushuka kutokana na uwekaji wa toni katika sibabi mbalimbali za maneno. Ikiwa sentensi ina maneno na silabi nyingi zinazodhihirisha kupanda na kushuka kwa nguvu zinazotumika katika utamkaji, basi itaathiri utoaji wa kiimbo katika Kiswahili kwa sababu inaonekana kuwa kupanda na kushuka kwa nguvu katika utamkaji kunapatikana katika sehemu chache katika Kiswahili. Kutouwepo kwa toni katika Kiswahili kunaifanya lugha hii kukosa kipengele kimoja ambacho kipo katika lugha ya Ekegusii. Kwa mujibu wa vipengele vya mfumo na utekelezaji vya NUKL2, huenda hali hii ya kupanda na kushuka kwa toni katika silabi moja ya kila neno ndiyo iliyosababisha athari hasi katika utamkaji wa kiimbo sahihi cha Kiswahili katika sentensi za amri na mshangao.

Wakaa katika Ekegusii na Kiswahili

Ni wakati unaotumiwa katika utamkaji wa foni (Massamba, 2004). Ni muda wa matamshi ya silabi moja ulio tofauti na umbo lingine linganifu kimuundo. Kuna aina tatu za wakaa. Wakaa wa kawaida, mfupi, na mrefu (Mgullu, 2010). Wakaa wa kawaida hutumia muda wastani, kwa upande mwingine wakaa mfupi hutumia muda mfupi katika utamkaji wa foni fulani ilhali ulio mrefu hutumia muda mrefu katika kutamka sauti fulani. Kwa maandishi ya kawaida, wakaa mrefu hudhihirisha kwa kurudia herufi lakini kuna ishara maalum ya kifonetiki yenye alama ya nukta mbili (:) ambayo huambatanishwa katika kilele cha silabi. Mgullu (keshatajwa), anaeleza kuwa wakaa unaweza kuwa wa kifonetiki au wa kileksia. Wakaa wa kifonetiki huwekwa mwishoni mwa silabi ili kukabiliana na kikwazo

cha matamshi sahihi kama vile inavyodhihirisha katika data 10

Data 10

Ukoo-uko:

Zubaa-zuba:

Katika (10), mzungumzaji akisema ‘uko’ badala ya ‘ukoo’, msikilizaji atabaini kuwa utamkaji una hitilafu wala maana haitapotea. Tofauti na wakaa wa kifonetiki, wakaa wa kileksia hubainisha maana za kimsingi. Ubainifu huu hudhihirika kupitia jozi ya maneno kama ilivyo katika data 11

Data 11

Poza/ po:za

Mchuzi/mchu:zi

Katika wakaa, kipimo kidogo cha muda wa kutamka sauti moja inayokadiriwa kuwa vokali au mseto wa konsonanti na vokali huitwa mora. Silabi yenye wakaa kwa kawaida huchukua muda wa mora mbili. Kuna baadhi ya wataalam amba wamechunguza wakaa katika lugha za Kibantu kama vile Hubbard (1995) aliyebaini kuwa vokali ndefu katika lugha ya CiTonga na Chichewa zina silabi mbili wala si mora mbili. Ingawa lugha ya Kiswahili haidhihirishi wizani wa silabi (Ntihirageza, 2001; Mwaliwa, 2014), huonyesha urefu wa vokali ndefu kwa silabi mbili. Park (1997) anatoa ushahidi kuhusu dosari iliyopo ya silabi za Kiswahili zinazochukuliwa kuwa zina vokali ndefu kwa kuwa kuna baadhi ya maneno ambayo yanaonyesha uwepo wa vokali fupi na ndefu kama inavyoonyeshwa katika (12).

Data 12

- a. Cha (kumiliki) b) chaa (aina ya samaki)
- Kuja (enda, fika) kujaa (kuwa nyingi)


Kutokana na mifano hii, vokali katika (a), ni fupi ilhali vokali zilizoko katika (b) zinatambuliwa kuwa ndefu kifonetiki. Hakuna tofauti katika utamkaji wala hali ya glota wakati wa kutamka vokali /a/ mara mbili. Katika Kiswahili hakuna tofauti za kifonetiki kati ya vokali ndefu na inayoandikwa mara mbili. Kwa upande wake,

Park (keshatajwa) anaeleza kuwa mfuatano huu wa irabu katika lugha ya Kiswahili unatokana na kudhoofika kwa konsonanti. Kama tulivyotaja awali, lugha ya Kiswahili pia inachukuliwa kuwa yenye futi ya trokee silabi ambapo uzani futi (kundi la silabi linalofuata ruwaza fulani ya uwekaji shadda) huwa na silabi mbili. Mojawapo ya silabi katika futi ndiyo huwekewa shadda kuanzia kulia hadi kushoto au kuanzia kushoto hadi kulia (Hayes, 1985). Maumbo haya ya vipashio vya kiarudhi yanayopangwa kwa futi pamoja na uwekaji wa shadda hubainisha mdundo wa lugha husika. Katika muktadha huu, kipashio cha kiarudhi kinachochukuliwa kuwa na vokali ndefu katika lugha ya Kiswahili huwa na vilele viwili ambavyo hukifanya kuwa silabi mbili

tofauti, moja ikiwa na muundo wa (KV) na nyingine (V). Katika neno ‘makaa’ kwa mfano, iwapo ‘kaa’ ingechukuliwa kama silabi moja pekee, basi shadda ingewekwa kwa silabi ‘ma’ kama muundo wa Kiswahili unavyoelekeza kuhusu uwekaji wa shadda. Hata hivyo, tunapata kuwa shadda iko kwenye ‘ka’ kumaanisha ‘kaa’ ni silabi mbili. Hii inatokana na kuwa katika lugha ya Kiswahili shadda huwekwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho wa kila neno husika. Ekegusii ina vokali ndefu ambayo huchukuliwa kuwa na mora mbili (Beale-Ravaya, 2022) ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili yenye vokali fupi zilizo na mora moja kama inavyoonyeshwa katika (13).

Data 13

Kielelezo 3: Tofauti ya Wakaa wa Kiswahili (a) na Ekegusii (b)



Kutokana na tofauti hizi za kumuundo, maneno yenye irabu ndefu katika sentensi za Kiswahili yatatakwa visivyo na wasailiwa wanaorudufu utekelezaji wa matamshi ya silabi ndefu ya Ekegusii kwa kuwa katika Kiswahili wizani wa silabi ndefu hautadhihirika kwa sababu kuna vina viwili. Kwa upande mwingine, wizani wa silabi ndefu katika lugha ya Ekegusii utadhihirika kwa sababu kuna kina kimoja chenye mora mbili katika irabu moja kama ilivyoonyeshwa katika mchoro wa (b). Hivyo basi, silabi nzito katika Ekegusii inadhihirisha futi yenye trokee ya ki-mora ambapo wizani wa silabi nzito huwa na kilele kimoja chenye mora mbili. Kwa mujibu wa

Perlmutter (1995), lugha zenyе tofauti kati ya vokali fupi na ndefu hudhihirisha tofauti katika wizani wa kifonolojia. Anapeana mfano wa Luganda wa neno ‘wela (kataa) na weela (pumzika). Mifano zaidi ya wakaa katika lugha ya Ekegusii ni kama ifuatayo;

Data 14

Ekegusii	Kiswahili
Iga	hivi
Igaa	hapa

aria	yale
aaria	mahali mbali

Tofauti katika vipengele vya kiarudhi na utekelezaji wake ambavyo vinajikita katika mihimili ya utekelezaji na semantiki, tunapata kuwa irabu za Ekegusii zinapoongezwa kwenye silabi yenye sifa sawa, hubadili kiimbo kuwa kirefu; vivyo hivyo hubadili maana ya neno. Mfano mzuri ni namna ilivyodhiihirishwa katika neno ‘iga’ lenye maana ya ‘hivi’ katika (14) ambalo ni tofauti na ‘igaa’ lililo na wakaa mrefu lenye maana ya ‘hapa’. Hivi ni kumaanisha kuwa silabi ikirefushwa hubadili maana ya neno husika. Kauli iyo hiyo itatolewa kwa neno ‘aria’ lenye maana ya ‘yale’ ambalo likiongezewa irabu /a/ mwanzoni huwa ‘aaria’ lenye maana ya ‘mahali mbali’. Athari ya wakaa wa Ekegusii kwa kiimbo cha Kiswahili ilidhihirika katika maneno mawili yaliyokuwa na irabu ndefu katika kifungu ambacho wasailiwa walipewa kusoma. Badala ya kusoma neno *msaada* kama ‘msa‘ada’ wasailiwa walilisoma kama ‘msaa‘da’. Katika Kiswahili kupanda kwa sauti hudhihirika katika kipashio ‘ada’, lakini katika Ekegusii kupanda kwa sauti hakukudhihirika katika kipashio ‘ada’ kwa sababu kilele cha irabu (a) kilitamkwa pamoja na konsonanti (s). Neno ‘maajabu’, ambalo pia lilikuwa kwenye kifungu kilichosomwa na wasailiwa liliufuata utaratibu uo huo.

Kutokana na haya, tunaona kuwa urefushaji wa vokali katika lugha ya Ekegusii unaweza kuleta tofauti katika maana ya maneno lakini hali hii ni tofauti katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa si lazima maneno yote yaliyo na wakaa mrefu kuwa na maana tofauti na wakaa wa kawaida. Katika maneno yenye irabu ndefu ya Kiswahili tuliyotaja, irabu moja haiwezi kuondolewa kwa kuwa hayatakuwa na maana yoyote. Hi ni tofauti na Ekegusii ambapo irabu moja katika maneno yenye irabu ndefu inaweza kudondolewa na bado yakabaki kuwa na maana. Tukitilia maanani kuwa Ekegusii ina irabu ndefu na fupi (Komenda na wenzake, 2013) huenda hii ndiyo sababu iliyochangia makosa katika kufasili kiimbo sahihi katika sentensi za Kiswahili. Hata hivyo, ni vizuri kutilia maanani kuwa ‘msaada’ na ‘maajabu’ ni

maneno ya kukopwa. Hili linaweza kuashiria kuwa ukopaji katika Kiswahili ni mojawapo ya athari za wakaa katika Kiswahili ambao huwatatiza wanafunzi wanaozungumza Ekegusii kama L1.

HITIMISHO

Makala hii imefafanua vipengele vya fonolojia arudhi ya Ekegusii vinavyoathiri kiimbo wakati wa kuzungumza Kiswahili sanifu. Imedhihirika kuwa lugha ya Ekegusii ina viarudhi vingine mbali na kiimbo ambavyo ni: shadda, toni na wakaa. Ijapokuwa Kiswahili pia kina shadda na wakaa katika mfumo wake, utekelezaji wa viarudhi hivi katika lugha hizi mbili una tofauti ambazo huchangua katika kuleta dosari katika matumizi ya kiimbo cha Kiswahili fasaha. Imebainika kuwa katika lugha ya Ekegusii, vokali zinapokuwa na wakaa mrefu, huwakilishwa kama vokali moja yenye mora mbili tofauti na Kiswahili ambapo vokali ndefu inachukuliwa kuwa vokali mbili zenyne vilele tofauti. Shadda inapowekwa kwenye kilele cha irabu, hii bila shaka itaadhiru utekelezaji wa vipengele vingine via kiarudhi ambavyo vinaathiri kiimbo. Ijapokuwa lugha hizi zina ukuruba katika utekelezaji wa shadda, kunazo tofauti bayana katika uwekaji shadda katika sentensi ya Ekegusii. Kwa vile kiimbo hubainika katika kiwango cha sentensi na virai (Massamba, 2012), haya yanaathiri kiimbo katika L2 ya wasailiwa. Tofauti kuu imebainika katika kipengele cha kimfumo ambapo Ekegusii kina toni ilhali Kiswahili hakina. Wasailiwa wanaozungumza L1 yenye toni wanatatizika kwenye kutumia kiimbo ipasavyo kwa L2 isiyo na toni kutokana na kurudufu jinzi wanavyotekelza kiimbo lengwa katika lugha yao ya kwanza. Kuna ushahidi kuwa uhawilisho wa viarudhi hivi kwa kiwango kikubwa huathiri matumizi sahihi ya kiimbo cha Kiswahili.

MAREJELEO

Barlow, A. R. (1960). *Studies in Gikuyu Grammar and idioms*. Edinburgh: Harvester Wheatshef.

- Batibo, H. (2017). Evolution of Tone in Bantu Languages. *Linguistic and Literary Broad Research and Innovation*, 6(2), 34-40.
- Beale-Rivaya, Y. (2022). *Ekegusii-Minority or minoritized language and cultures*. NEH Distinguished Professor. Texas State University.
- Corder, S. (1967). *Error Analysis and Interlanguage*. Oxford University Press.
- Durand, V. (1990). *Severe Behavior problems: A functional Training Approach*. New York: Guilford press.
- Goldsmith, J. (1990). *Autosegmental and Metrical Phonology*. Oxford: Basil Blackwell.
- Hayes, B. (1985) Iambic and Trochaic Rhythm in Stress Rules. *Proceedings of the Eleventh Annual Meeting of the Berkeley Linguistics Society*, 429-446.
- Hubbard, K. (1995). 'Prenasalised consonants' and syllable timing: evidence from Runyambo and Luganda. *Phonology*, 12(2), 235-256.
- Hyman, L. M. (1975). Phonology: theory and analysis. (*No Title*).
- Janda, R & Auger, J. (1992). Quantitative evidence, qualitative hypercorrection, sociolinguistic Variables And French speakers' eadhaches with english h/Ø. *Language & Communicafion* 12, 3/4 (195-236).
- Khvtisiashvili, T. (2018). Phonological processes, transfer, and markedness. *The TESOL encyclopedia of English language teaching*, 1-6.
- Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA): Sekondari na vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- Komenda, S., Maroko, G.M., & Ndung'u, R.W. (2013). The morphophonemics of vowel compensatory lengthening in Ekegusii. *International Journal of Education and Research*, 1(9), 1-16
- Labov, W. (1966). Hypercorrection by the lower middle class as a factor in linguistic change. *Sociolinguistics. The Hague: Mouton*, 84(10).
- Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lughya*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D. P. B. (2012). *Misingi ya Fonolojia*. Dar es salaam: TUKI.
- Mennen, I. (2004). Bi-directional Interference in the Intonation of Dutch Speakers of Greek. *Journal of Phonetics*, 32, 543-563.
- Mennen, I. (2007). Phonological and phonetic influences in non-native intonation. *Non-native prosody: Phonetic descriptions and teaching practice*, 53-76.
- Mennen, I. (2015). Beyond segments: Towards a L2 intonation learning theory. In *Prosody and language in contact: L2 acquisition, attrition, and languages in multilingual situations* (pp. 171-188). Berlin, Heidelberg: Springer Berlin Heidelberg.
- Mennen, I., Reubold, U., Endes, K., & Mayr, R (2022). Plasticity of native intonation in the L1 of English migrants to Austria. *Language*, 7(3), 1-27.
- Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu: fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publisher
- Mgullu, R. (2010). *Mtalaa wa Isimu: fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publisher
- Mogaka, R. (2009). *Fonolojia ya utohozi wa maneno mkopo ya Ekegusii kutoka Kiswahili*. Tasnifu isiyochapishwa ya M.A. Chuo kikuu cha Kenyatta.

- Mose, E. G. (2020). A morphophonological analysis of borrowed segments in Ekegusii language: An Optimality Perspective. *Unpublished PhD thesis, Kenyatta University, Nairobi, Kenya.*
- Mwaliwa, H. C. (2014). *An analysis of the syllable Structure of Standard Kiswahili loanwords from Modern Standard Arabic* (Doctoral dissertation).
- Nandelenga, H. S. (2015). The Lubukusu syllable structure in optimality theory in Phonology. *The international journal of Humanites and Social studies*, 3(3), 86-10.
- Nash, C. M. (2011). *Tone in Ekegusii: A description of nominal and verbal tonology*. University of California, Santa Barbara.
- Ntihirageza, J. (2001). Quantity Insensitive in Bantu Languages. *Unpublished PhD Dissertation. University of Chicago.*
- Obara, J. M. (2014). *Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Osinde, K. N. (1988). *EkeGusii morphophonology: An analysis of the major consonantal processes* (Doctoral dissertation, University of NAIROBI).
- Park, J. I. (1997). *Minimal word effects with special reference to Swahili*. Indiana University.
- Perlmutter, D. (1995). Phonological quantity and multiple association. *The Handbook of Phonological Theory*. Oxford: Blackwell, 307-17.
- Roach, P. (1983). *English phonetics and phonology: A practical course*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Son, J. (2018). *Acquisition of Spanish intonation by Native Korean speakers*. University of California, Los Angeles.
- Vâlcea, C. S. (2020). First language transfer in second language acquisition as a cause for error-making in translations. *Diacronia*, (11), 1-10. DOI: <http://dx.doi.org/10.17684/i11A161en>
- Welmers, W.E. (1973). African Language structure. Berkeley: University of California Press.
- Yip, M. (2002) Tone. Cambridge. Cambridge university press